NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU
Riḍván 2021

Kwa Wabahá'í wa Ulimwengu
Marafiki Wapendwa sana,

1. Maneno ya mwisho katika sura ikumbukwayo mno katika historia ya Hoja sasa yameandikwa, na ukurasa umegeuzwa. Riḍván hii huashiria hitimisho la mwaka usio wa kawaida, wa Mpango wa Miaka Mitano, na wa mfululizo mzima wa Mipango ambayo ilianza mnamo mwaka 1996. Mfuatano mpya wa Mipango unatoa ukaribisho, kwa kile kinachotumainiwa kuwa ni miezi kumi na mbili yenye maana sana ikitumika kama utangulizi wa jitihada za miaka tisa zinazotarajiwa kuanza Riḍván ijayo. Sisi tunaiona mbele yetu jumuiya ambayo imepata nguvu kwa kasi na ipo tayari kupiga hatua kubwa kubwa kusonga mbele. Lakini sharti pasiwepo na fikra za udanganyifu kuhusu kiwango cha juhudi kilichohitajika kufika mahali hapa na umaizi wa hali ya juu kiasi gani ulipatikana njiani: masomo tuliyojifunza ndiyo yataumba muskakabali wa jumuiya, na maelezo ya jinsi yalivyopatikana hutoa mwanga juu ya kinachotarajiwa.

2. Miongo iliyotufikisha mwaka 1996, ikiwa na utajiri wa maendeleo na umaizi wa kwayo yenyewe, haikuacha shaka kwamba idadi kubwa ya watu katika jamii nyingi wangekuwa tayari kuingia chini ya bendera ya Imani. Walakini, japokuwa matukio ya uandikishaji mkubwa yalikuwa ya kuhamasisha, hayakulingana na mchakato wa ukuaji uliosarifiwa ambao ungeweza kulelewa katika mazingira mbalimbalii. Maswali ya kina yaliikabili jumuiya, ambayo, wakati huo, haikuwa na uzoefu wa kutosha kuyajibu ipasavyo. Ingewezekanaje juhudi zilizokusudiwa kwenye upanuzi wake kusonga mbele bega kwa bega na mchakato wa uimarishaji na kutatua changamoto za muda mrefu ambazo zilionekana kuwa sugu katika kudumisha ukuaji? Ingewezekanaje watu binafsi, asasi na jumuiya kuinuliwa ambao wangeweza kutafsiri mafundisho ya Bahá'u'lláh katika vitendo? Na ingewezekanaje wale waliovutiwa kwenye mafundisho kuwa wahusikka wakuu katika juhudi ya kiroho ya ulimwengu?

3. Kwa hiyo ilikuwa kwamba, katika robo karne iliyopita, jumuiya ya Kibahá'í ambayo ilikuwa ikijihesabia Mikono wa Hoja ya Mungu watatu katika safu zake za mbele, kuingia katika Mpango wa Miaka Minne, uliojipambanua kutoka ile iliyokuja kabla yake kwa kumakinikia shabaha moja: hatua ya maana katika mchakato wa uingiaji kwa makundi. Shabaha hii ilikuja kuainisha mfuatano wa Mipango ambayo ilifuata. Jumuiya tayari ilikuwa imeelewa kwamba mchakato huu haukuwa tu kwa ajili ya uingiaji katika Imani kwa makundi makubwa, wala hilo halingejitokeza tu; ulimaanisha kusudio, mpangilio, uchapuzaji wa upanuzi na uimarishaji. Kazi hii ingehitaji ushiriki utambulikao wa roho nyingi kuu, na mnamo mwaka 1996, ulimwengu wa Kibahá'í uliitwa kubeba changamoto kubwa ya kielimu ambayo hii hujumuisha. Iliitwa kuanzisha mtandao wa taasisi za mafunzo wenye shabaha ya kuzalisha mtiririko uongezekao wa watu binafsi waliojaaliwa vipaji vinavyohitajika kudumisha mchakato wa ukuaji.

4. Marafiki walianza kazi hii wakitambua kwamba, licha ya ushindi wao wa nyakati zilizopita katika nyanja za ufundishaji, ilikuwa dhahiri kuwa walikuwa na mengi ya kujifunza kuhusu uwezo uliohitajika na, kikubwa zaidi, jinsi ya kuupata. Kwa namna nyingi, jumuiya ingejifunza kwa vitendo, na masomo iliyojifunza, mara baada ya kuchujwa na kuboreshwa kwa kutumika katika mazingira mbalimbali kadiri muda unavyopita, hatimaye yangejumuishwa katika nyenzo za kielimu. Ilitambulika kwamba baadhi ya shughuli zilikuwa matokeo ya kawaida kwa mahitaji ya kiroho ya umma. Vikundi vya mafunzo, madarasa ya watoto, mikutano ya ibada, na baadaye vikundi vya vijana chipukizi zilijitokeza kama viini muhimu katika muktadha huu, na vilipofumwa pamoja na shughuli zinazohusiana, nguvu zilizozalishwa zilianzisha ruwaza yenye msisimko ya maisha ya jumuiya. Na kadiri idadi ya wanaoshiriki katika shughuli za msingi ilivyokua, kipimo kipya kiliongezwa kwenye kusudi la mwanzo. Shughuli hizi zilikuja kuwa milango ambayo kupitia humo, vijana, watu wazima na familia nzima kutoka jamii pana zaidi waliweza kuja kukutana na Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Pia ilikuwa inajitokeza dhahiri, jinsi gani kiuhalisia ilivyofaa kufikiria mikakati ya kazi ya ujenzi wa jumuiya katika muktadha wa "klasta": eneo la kijiografia ambalo linaoweza kusimamiwa ikiwa na sura dhahiri za kijamii na kiuchumi. Uwezo wa kuandaa mipango rahisi kwenye ngazi ya klasta ulianza kukuzwa, na kutokana na mipango kama hiyo, programu kwa ajili ya ukuaji wa Imani ziliibuka, zikipangwa katika kile ambacho kilikuja kujwa maduru ya miezi mitatu mitau ya shughuli. Kipengele muhimu bayana kiliibuka mapema kwenye: mjongeo wa watu binafsi kupitia mlolongo wa kozi unaoupa msukumo, na kuendelezwa na, mjongeo wa klasta katika mwendelezo wa maendeleo. Uhusiano huu unaokamilishana uliwasaidia marafiki kila mahali kupima mienendo ya ukuaji katika maeneo yao wenyewe na kutengeneza njia kuelekea kwenye nguvu zilizoongezeka. Kadiri muda ulivyopita, ilithibitika ni jambo lenye manufaa kuona kile kilichokuwa kikitokea katika klasta, kwa pande zote mbili, kutoka mtazamo wa mambo matatu muhimu ya kielimu—kuwahudumia watoto, vijana chipukizi, na vijana na watu wazima—halikadhalika kutoka mtazamo wa maduru ya shughuli muhimu kwenye wizani wa ukuaji. Wakati hayo yakiendelea ndani ya jitihada ya miaka ishirini na tano, sehemu kubwa ya sura zinazotambulika za mchakato wa ukuaji, leo tunaziona zikiwa zinaimarishwa vyema.

5. Kadiri jitihada za marafiki zilivyoshadidishwa, kanuni mbalimbali, dhana na mikakati ifaayo kote ulimwenguni kwa mchakato wa ukuaji ilianza kupata umbo kama muundo kwa ajili ya vitendo ambavyo vingebadilika kupokea vipengele vipya. Muundo huu ulithibitika kuwa wa msingi kwa ajili ya uachiliaji wa nguvu kubwa mno. Uliwasaidia marafiki kuelekeza nguvu zao katika njia ambazo tajiriba ilionesha kuwa zinafaa kwa ukuaji wa jumuiya yenye hali njema. Lakini muundo siyo kanuni. Kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya muundo wakati wa kupima uhalisia wa klasta, eneo au ujirani tu, ruwaza ya shughuli ingeweza kukuzwa ambayo ingechota kutoka kile ambacho sehemu zingine za ulimwengu wa Kibahá'í zilikuwa zinajifunza zilipokuwa zikijibu mambo husika ya vipengele vya mahali hapo. Uwili kinzani kati ya mahitaji ya lazima kwa upande mmoja na chaguo binafsi zisizo na ukomo kwa upande mwingine vilitoa njia kwa uelewa tofauti mdogo zaidi wa njia mbalimbali ambazo kwazo watu binafsi wangeweza kuunga mkono mchakato ambao, kwenye kiini chake, ulikuwa sambamba na unaoendelea kuboreshwa kadiri tajiriba ilivyokusanywa. Hebu pasiwe na shaka yoyote kuhusu maendeleo yanayowakilishwa na uibukaji wa muundo huu**:** athari za kupatanisha na kuunganisha

jitihada za ulimwengu mzima wa Kibahá'í na kusukuma mwendo wake kwenda mbele zilikuwa za matokeo makubwa.

6. Kadiri Mpango mmoja ulivyourithi mwingine, na uhusikaji na kazi za ujenzi wa jumuiya ulivyokuwa na msingi mpana zaidi, maendeleo kwenye ngazi ya kitamaduni yalionekana zaidi. Mathalani, umuhimu wa uelimishaji wa kizazi kichanga zaidi, ulikubalika kwa mapana zaidi, kama ambavyo uwezo usio wa kawaida uliowakilishwa hasa na vijana chipukizi. Roho zikisaidiana na kuambatana kwa pamoja kwenye njia moja, daima ziliendelea kupanua duara la kuhimiliana, zikawa mtindo ambao nguvu zote zilielekezwa kwenye ujengaji wa uwezo kwa huduma iliyotarajiwa. Hata mwingiliano wa marafiki miongoni mwao wenyewe na pamoja na wale wanaowazunguka ulipitia mabadiliko, kadiri utambuzi ulivyoinuliwa kuhusu nguvu ya maongezi yenye maana kuwasha na kuchochea hisia za kiroho. Na kwa umuhimu, jumuiya za Kibahá'í zilijitwalia mwelekeo uliozidi kutazama nje. Roho yoyote iliyokuwa pokevu kwa muono wa Imani ingeweza kuwa mshiriki hai—hata mwendelezaji na mraghibishaji—wa shughuli ya kielimu, mikutano kwa ajili ya ibada na vipengele vingine vya kazi za ujenzi wa jumuiya; kutoka miongoni mwa roho kama hizo, wengi pia wangejitangaza imani yao kwa Bahá'u'lláh. Hivyo, wazo la mchakato wa uingiaji kwa makundi liliibuka ambalo kidogo lilitegemea juu ya nadharia na mawazo na zaidi juu ya tajiriba halisi ya jinsi idadi kubwa ya watu ingeweza kuipata Imani, kuifahamu, kujitambulisha na shabaha zake, kujiunga na shughuli na majadaliano yake, na mara nyingi kuipokea. Kwa kweli, kadiri mchakato wa taasisi ulivyoimarishwa katika eneo hadi eneo, idadi ya watu binafsi waliochukua sehemu ya kazi ya Mpango, ikiwafikia hata wale walioijua Imani hivi karibuni, ilikua kwa upesi mno. Lakini hii haikuwa inasukumwa tu na wasiwasi wa idadi. Muono wa mabadiliko ya mtu binafsi na ya pamoja yakitokea sanjari, juu ya msingi wa ujifunzaji wa Neno la Mungu na utambuzi wa uwezo wa kila mtu wa kuwa muhusika mkuu katika igizo la kina la kiroho, uliibua hisia ya juhudi za pamoja.

7. Mojawapo ya sura za kuvutia na kuhamasisha katika kipindi hiki cha miaka ishirini na tano imekuwa huduma iliyotolewa na vijana wa Kibahá'í, ambao kwa imani na ushujaa wamechukua nafasi zao halali kwenye safu za mbele katika jitihada za jumuiya. Kama walimu wa Hoja na waelimishaji wa vijana, kama wakufunzi wasafiri na watangulizi wa ndani, kama waratibu wa klasta na wajumbe wa wakala za Kibahá'í, vijana katika mabara matano wameinuka kuhudumia jumuiya zao kwa kujitoa na dhabihu. Ukomavu waliouonesha, katika kutekeleza majukumu ambayo juu yake yanategemea maendeleo ya Mpango Mtakatifu, ni huelezea uhai wao wa kiroho na kujifunga kwao ili kuulinda mustakabali wa jamii ya wanadamu. Kwa kutambua ukomavu huu unaoendelea kudhihirika, tumeamua kwamba, mara baada ya Riḍván hii, wakati umri wa muumini anayestahili kuchaguliwa kuhudumu katika Baraza la Kiroho utabakia miaka ishirini na moja, umri wa muumini anayeweza kupiga kura katika uchaguzi wa Kibahá'í unashushwa hadi kufikia miaka kumi na nane. Sisi hatuna shaka kabisa kwamba vijana wa Kibahá'í kila mahali ambao wametimiza umri huo, watathibitisha kuwa uamuzi wetu ni sahihi kwa kuamini uwezo wao wa kutimiza kwa 'utambuzi na kwa bidii' 'jukumu takatifu' ambalo kila Mbahá'í mpiga kura anaitiwa.

*

8. Tunatambua kwamba, kwa kawaida uhalisia wa jumuiya hutofautiana kwa kiasi kikubwa. Jumuiya mbalimbali za kitaifa, na sehemu tofauti tofauti ndani ya jumuiya hizo, zilianza mfuatano huu wa Mipango katika hatua tofauti tofauti za maendeleo; tangu hapo, pia wameendelea kukua kwa kasi tofauti tofauti na kufikia viwango tofauti tofauti vya maendeleo. Hili lenyewe, siyo jambo jipya. Daima imekuwa hivyo kwamba hali katika sehemu mbalimbali hutofautiana, kama vile kinavyo tofautiana kiwango cha upokevu kinachopatikana hapo. Lakini tunaliona, vile vile, wimbi linalotutumka, ambalo kwalo uwezo, kujiamini na tajiriba zilizokusanywa za jumuiya nyingi zinainuka, zikichelezwa na mafanikio ya jumuiya dada za karibu na mbali. Kama mfano, wakati roho zilizoinuka kufungua maeneo mapya mnamo mwaka 1996 hazikupungukiwa na chochote katika ujasiri, imani na kujitoa, leo wenzao kila mahali wanachanganya sifa hizo hizo pamoja na ujuzi, umaizi na weledi ambavyo ni matokeo ya mkusanyiko wa jitihada za miaka ishirini na tano zilizofanywa na ulimwengu mzima wa Kibahá'í kupangilia na kuboresha kazi za upanuzi na uimarishaji.

9. Bila kujali ni wapi jumuiya huanzia, imeendeleza mchakato wa ukuaji pale ilipochanganya sifa za imani, ustahimilivu na kujidhatiti na utayari wa kujifunza. Kwa kweli, urithi tuupendao mno wa mfuatano huu wa Mipango ni utambuzi ulioenea kwamba jitihada yoyote ya kupiga hatua huanza na mwelekeo wa kujifunza. Urahisi wa mwongozo huu humezwa na maana ya athari zinazotokana nao. Sisi hatuna shaka kwamba kila klasta, ikipewa muda, itapiga hatua kwenye mwendelezo wa maendeleo; jumuiya ambazo zimeendelea kwa haraka zaidi, zikilinganishwa na zile ambazo hali zao na uwezekano vilifanana, zimeonesha uwezo wa kulea umoja wa fikra na kujifunza kuhusu utendaji unaofaa. Na zilifanya hivyo bila kusita kutenda.

10. Kujifunga kibwewe kwa ajili ya kujifunza pia kulimaanisha kuwa tayari kufanya makosa—na wakati mwingine, bila shaka, makosa yalileta adha. Haikushangaza, kuwa hapo mwanzoni mbinu na njia mpya zilitumika bila ustadi mkubwa kwa sababu ya ukosefu wa tajiriba; wakati mwingine, uwezo wa aina moja uliopatikana karibuni ulipotea kwani jumuiya ilijishughulisha na ukuzaji wa uwezo mwingine. Kuwa na nia nzuri kabisa siyo uhakika wa kutokosea hatua, na kusonga mbele tukiyapita hayo huhitaji yote mawili unyenyekevu na kujitenga. Pale ambapo jumuiya imebakia iliyodhamiria kuonesha ustahimilivu na kujifunza kutokana na makosa ambayo hutokea kwa kawaida, kuyafikia maendeleo kamwe hakujawahi kukwama.

11. Katikati ya mfuatano wa Mipango, ujihusishaji wa jumuiya katika maisha ya jamii ulianza kuwa shabaha ya umakinifu wa moja kwa moja. Waumini walihamasishwa kulifikiria hili katika muktadha wa maeneo mawili unganifu ya jitihada—vitendo vya kijamii na ushiriki katika mijadala iliyoenea ya kijamii. Haya, bila shaka, hayakuwa mbadala kwa kazi ya upanuzi na uimarishaji, wala kutuvuruga kutoka kazi hii: kiasili zilikuwa ndani yake. Kadiri ilivyokuwa kubwa zaidi rasilimali watu ambayo jumuiya ingeihitaji, ndivyo ulivyokuwa mkubwa zaidi uwezo wa kuleta hekima iliyomo katika Ufunuo wa Bahá'u'lláh wa kukabiliana na changamoto za siku—kutafsiri mafundisho Yake katika uhalisia. Na masuala yenye kusumbuliwa ya jamii ya wanadamu ya wakati yalionekana kutilia mkazo juu ya jinsi gani ilivyohitajika mno tiba iliyoagizwa na Tabibu Mtakatifu. Kilichomaanishwa katika haya yote lilikuwa ni wazo la dini tofauti sana kutoka zile zinazoshikilia ulimwengu mpana unaoyumba: wazo ambalo lilitambua dini kuwa kani

yenye uwezo unaosukuma ustaarabu uendeleao mbele daima. Ilieleweka kuwa ustaarabu kama huo usingejitokeza tu hivi hivi kwa uwezo wake wenyewe—ilikuwa ni dhima ya wafuasi wa Bahá'u'lláh kufanya kazi kwa ajili ya uibuka wake. Dhima kama hiyo ilidai mchakato ule ule wa ujifunzaji wa utaratibu kwa ajili ya kazi ya vitendo vya kijamii na kujihusisha katika mijadala ya hadhara.

12. Ikiangaliwa kutoka mtazamo wa miongo miwili na nusu iliyopita, uwezo wa kufanya vitendo vya kijamii umeongezeka sana, ukipelekea kwenye uchanuaji usio wa kawaida wa shughuli. Ikilinganishwa na mwaka 1996, ambapo miradi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi takriban 250 ilikuwa ikidumishwa kutoka mwaka hadi mwaka, sasa ipo 1,500; na idadi ya mashirika yenye msukumo wa Kibahá'í yameongezeka mara nne kupita 160. Zaidi ya jitihada 70,000 za vitendo vya kijamii mashinani vya vipindi vifupi vinafanyika kila mwaka, ongezeko la mara hamsini. Tunatarajia ongezeko linaloendelea la jitihada zote hizi zinazotokana na uungwaji mkono wa dhati na uchocheaji unaotolewa sasa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Kibahá'í. Wakati huo huo, ushiriki wa Wabahá'í katika mijadala ya kijamii inayoendelea pia imekua sana. Licha ya matukio mengi ambapo marafiki wanaona wanaweza kutoa mtazamo wa Kibahá'í katika maongezi yanayotokea katika kazi au katika muktadha wa mtu binafsi, ushiriki rasmi zaidi katika maongezi umeongezeka sana. Akilini siyo tu tunazo, siyo tu jitihada zilizopanuliwa mno na michango inayoendelea kuwa ya kisasa kutoka Jumuiya ya Kimataifa ya Kibahá'í—ambayo katika kipindi hiki imeongeza Ofisi Afrika, Asia na Ulaya—lakini pia kazi za mtandao ulioongezwa kwa kiasi kikubwa na kuimarishwa sana wa Ofisi za kitaifa za Mambo ya Nje, ambao kwazo eneo hili la jitihada limekuwa shabaha kuu; na zaidi, ilikuwepo michango yenye umaizi na ionekanayo iliyofanywa na waumini binafsi kwa maeneo maalum. Yote haya yanapelekea kueleza taadhima, uthamini na kupendezwa ambavyo viongozi wa fikra na watu wengine mashuhuri kutoka ngazi zote za jamii wamezionesha tena na tena kwa ajili ya Imani, wafuasi wake na shughuli zao.

13. Katika kupitia kipindi chote cha miaka ishirini na tano tunashangazwa na maendeleo ya aina nyingi ambayo ulimwengu wa Kibahá'í umeyafanya kwa pamoja. Uhai wake wa kiakili umeshamiri, kama ilivyooneshwa siyo tu kwa maendeleo yake katika maeneo yote ya jitihada ambayo yameshaongelewa, lakini pia kwa wingi wa machapisho yenye ubora ambayo yamechapishwa na watunzi wa Kibahá'í, kwa kukuza nafasi kwa ajili ya uchunguzi wa baadhi ya taaluma kufuatana na mafundisho, na athari ya wanachuo na semina za wanafunzi zilizotolewa na Taasisi ya Mafunzo kwa ajili ya Ustawi wa Ulimwengu, ambayo, kwa ushirikiano na asasi za Hoja, sasa inawahudumia vijana wa Kibahá'í kutoka zaidi ya nchi 100. Jitihada za kujenga Nyumba za Ibada zimechapuzwa kwa uwazi kabisa. Hekalu Mama la mwisho lilijengwa huko Santiago, Chile, na miradi ya kujenga Hekalu mbili za kitaifa na Mashriqu'l-Adhkár tano za mahali ilianzishwa; Nyumba za Ibada za Battambang, Kambodia, na Norte del Cauca, Colombia, tayari zimeshafungua milango yake. Hekalu za Kibahá'í, ziwe mpya zilizozinduliwa au zilizojengwa zamani, zinaendelea zaidi na zaidi kuchukua nafasi katika moyo wa maisha ya jumuiya. Msaada wa nyenzo unaotolewa na safu za waumini kwa ajili ya jitihada lukuki zinazofanywa na marafiki wa Mungu umekuwa usio na uchoyo. Ikiangaliwa tu kama kipimo cha uhai wa pamoja wa kiroho, ukarimu na dhabihu ambavyo, katika kipindi cha ghasia nyingi za kiuchumi, mtiririko muhimu wa fedha umeweza kuendelezwa—la, kuongezewa nguvu zaidi—unajieleza sana. Katika milki ya utawala wa Kibahá'í, uwezo wa Mabaraza ya

Kiroho ya Kitaifa kusimamia masuala ya jumuiya zao katika utata wao unaokua, umeongezeka kwa kiwango kikubwa. Wamenufaika husani kutoka vilele vipya vya ushirikiano na Washauri, ambao wamekukuwa chombo katika kupangilia ukukusanyaji wa umaizi kutoka mashinani kote ulimwenguni na kuhakikisha usambazwaji wake kwa mapana. Hiki pia kilikuwa kipindi ambamo Halmashauri za Kibaha'i za Kanda ziliibuka kama asasi kamili ya Hoja, na katika majimbo 230 sasa, Halmashauri na zile taasisi za mafunzo wanazozisimamia zimejithibitisha zenyewe kuwa za lazima kwa ajili ya uendelezaji wa mchakato wa ukuaji. Kuendeleza kazi za Mdhamini Mkuu wa Ḥuqúqu'lláh, Mkono wa Hoja ya Mungu 'Alí-Muḥammad Varqá, Bodi ya Kimataifa ya Wadhamani wa Ḥuqúqu'lláh ilianzishwa mnamo mwaka 2005; leo inaratibu juhudi zisizopungua 33 kitaifa na Bodi za Wadhamini za Kanda ambazo sasa zinazingira ulimwengu mzima; ambazo zenyewe huongoza kazi ya Wawakilishi zaidi ya 1,000. Maendeleo yaliyotokea Makao Makuu ya Kibahá'í ya Ulimwengu katika kipindi hiki hiki katika ni mengi: tulishuhudia kukamilika kwa Ngazi ya Kaburi la Báb na majengo mawili juu ya Tao, na mwanzo wa ujenzi wa Kaburi la 'Abdu'l-Bahá, bila kusahau kutaja miradi mingi ya kuongeza nguvu na kuhifadhi Maeneo Mtakatifu yenye thamani ya Imani. Kaburi la Bahá'u'lláh na Kaburi la Báb yalitambulika kama maeneo ya Urithi wa Ulimwengu, sehemu zenye umuhimu usiokadirika kwa wanadamu. Umati ulikusanyika kwenye sehemu hizi takatifu kwa mamia ya maelfu, takriban milioni moja na nusu katika baadhi ya miaka, na Kituo cha ulimwengu kila mara kiliwakaribisha mamia ya mahujaji kwa wakati mmoja, wakati mwingine zaidi ya 5,000 kwa mwaka, pamoja na idadi kama hiyo ya wageni wa Kibahá'í; tunafurahi sana kwa idadi iliyoongezeka sawa na korija za watu tofauti tofauti na mataifa yanayowakilishwa miongoni mwa wale wanaojaliwa kuhiji. Tafsiri, machapisho na usambazaji wa Vitabu Vitakatifu pia vimechapuzwa kwa kiwango kikubwa, sambamba na maendeleo ya Maktaba ya Marejeo ya Kibahá'í, mojawapo ya wajumbe watambulikao wa familia inayokua ya tovuti zinazohusiana na tovuti ya Bahai.org, ambayo yenyewe sasa inapatikana katika lugha kumi. Ofisi mbalimbali na wakala zimefunguliwa, katika Makao Makuu ya Ulimwengu na mahali penginepo, zikiwa zimepewa kazi ya kusaidia mchakato wa ujifunzaji ambao unaendelea kukunjuka katika maeneo mengi ya jitihada kila mahali katika ulimwengu wa Kibahá'í. Dada zetu na kaka zetu katika imani, yote haya, ni sehemu ndogo tu ya kisa ambacho tunaweza kusimulia kuhusu kile kilicholetwa na kujitolea kwenu kwa Yule Ambaye alikuwa Mdhulumiwa wa ulimwengu. Tunaweza kurudisha mwangwi tu wa maneno yenye hisia yaliyosemwa wakati mmoja na mpendwa Bwana pale alipozidiwa na hisia, Yeye alisema kwa sauti: "Ee Bahá'u'lláh! Umefanya nini Wewe?"

14. Kutoka mfululizo wa taswira ya maana sana ya robo karne, sasa tunaelekeza macho yetu kwenye Mpango wa Miaka Mitano wa hivi karibuni kabisa, Mpango ambao ni tofauti kabisa na wowote uliopita hapo awali kwa namna mbalimbali. Katika Mpango huu tumewasihi Wabahá'í wa ulimwengu kuyachukua yale yote waliyojifunza kwa miaka ishirini iliyopita na kuyaweka katika matumizi kamilifu. Tumefurahishwa kwamba matumaini yetu kuhusu jambo hili yalitimizwa zaidi ya matarajio, lakini wakati kwa kawaida tungetarajia mambo makubwa kutoka kwa wafuasi wa Uzuri Uliobarikiwa, hulka ya kile kilichopatikana kupitia jitihada zao zilizohitaji nguvu nyingi hakika ilikuwa ya kustaajabisha. Ilikuwa ni kilele kwa mafanikio ya miaka ishirini na tano inayoendelea kujengeka.

15. Hususan Mpango ulikuwa wa kukumbukwa kwa kugawanywa sehemu tatu kwa maadhimisho mawili matakatifu ya miaka mia mbili, kila moja ikizichagiza jumuiya za mahali kote ulimwenguni. Kikosi cha waaminifu kilionesha kwa kiwango ambacho hakijawahi kushuhudiwa hapo awali na kwa urahisi ulioje, uwezo wa kuwashirikisha watu kutoka sehemu zote za kijamii kwa ajili ya kuyaenzi maisha ya Mdhihirishaji wa Mungu. Ilikuwa ishara yenye nguvu ya kitu kipana zaidi: uwezo wa kuelekeza nguvu za ajabu za kiroho zilizoachiliwa kwa ajili ya maendeleo ya Hoja. Mwitikio ulikuwa adhimu mno kiasi kwamba katika maeneo mengi Imani ilisukumwa kutoka katikati ya giza la kutojulikana hadi kwenye ngazi ya kitaifa. Katika mazingira ambapo haikutarajiwa, labda haikutazamiwa, upokevu wa kutambulika kwa Imani ukawa dhahiri. Maelfu kwa maelfu kwa maelfu walifikishwa mbali kwa kukutana na moyo ya kiibada ambao leo unaiainisha jumuiya ya Kibahá'í kila mahali. Muono wa kile kilichofanywa kiwezekane kwa kuadhimisha Siku Takatifu za Kibahá'í ulipanuliwa kwa kiasi kisichopimika.

16. Mafanikio ya Mpango, hata kwa namna ya tarakimu tu, kwa haraka umeyafunika kwa mbali sana yale ya Mipango yote ambayo imeutangulia tangu mwaka 1996. Mwanzoni mwa Mpango huu, kulikuwa na uwezo wa kuendesha shughuli za msingi zaidi ya 100,000 hivi ndani ya muda fulani, uwezo ambao ulikuwa ni matunda ya jitihada ya pamoja ya miaka ishirini. Sasa, shughuli za msingi 300,000 zinadumishwa kwa wakati mmoja. Ushiriki katika shughuli hizo umepanda kupita milioni mbili, ambao pia ni takriban ongezeko la mara tatu. Kuna taasisi 329 za mafunzo za kitaifa na kanda zinazotenda kazi, na uwezo wao umeshuhudiwa na ukweli kwamba robo tatu ya watu milioni moja wamewezeshwa kumaliza angalau kitabu kimoja cha mlolongo; kwa jumla, idadi ya kozi ambazo mtu binafsi amemaliza sasa pia ni milioni mbili—ongezeko zuri zaidi la mara tatu katika miaka mitano.

17. Nguvu iliyoongezeka ambayo inatumiwa na programu za ukuaji zinazofanyika kote ulimwenguni, inatuambia kisa cha aina yake cha kuvutia. Katika kipindi hiki cha miaka mitano, tulitoa wito wa kuchapuzwa ukuaji katika kila moja ya klasta 5,000 ambako ilikuwa imeanzia. Agizo hili likawa msukumo kwa ajili ya jitihada za dhati kote ulimwenguni. Kama matokeo, idadi ya programu shadidi za ukuaji ziliongezeka maradufu na sasa zipo takriban 4,000. Matatizo yaliyohusika katika kufungua vijiji vipya na ujirani kwa ajili ya Imani katikati ya janga la kiafya la kiulimwengu, au kupanua shughuli ambazo zilikuwa kwenye hatua za mwanzo wakati janga lilipoanza, yalizuia hata ufikiwaji wa jumla wa idadi ya juu zaidi wakati wa mwaka wa mwisho wa Mpango. Hata hivyo, yapo mengine ya kusimulia zaidi ya haya. Mwanzoni mwa Mpango, tulieleza matumaini yetu kwamba idadi ya klasta ambako marafiki wangekuwa wamepita hatua ya tatu kwenye mwendelezo wa ukuaji, kama matokeo ya ujifunzaji jinsi ya kukaribisha idadi kubwa katika kukumbatia shughuli zao, ingeendelea kukua kwa mamia zaidi. Jumla hiyo wakati ule ilikuwa takriban kwenye 200, iliyoenea katika kiasi cha nchi 40. Miaka mitano kuendeelea, imefikia idadi ya kustaajabisha ya 1,000 katika takriban nchi 100—robo ya programu zote za ukuaji shadidi ulimwenguni na mafanikio yanayopita sana matarajio yetu. Na bado hata idadi hizi hazioneshi vilele vya juu kabisa ambako jumuiya imefikia. Zipo zaidi ya klasta 30 ambako idadi ya shughuli za msingi zinazodumishwa zinazidi 1,000; mahali pengine, jumla ni maelfu kadhaa, zikihusisha ushiriki wa zaidi ya watu 20,000 katika klasta moja. Idadi inayoendelea kukua ya Mabaraza ya Kiroho ya Mahali sasa inasimamia ukunjukaji wa programu za kielimu zinazohudumia takriban watoto na vijana chipukizi wote katika

kijiji; uhalisi huo huo unaanza kuibuka ndani ya viunga vichache vya mijini. Kujihusha na Ufunuo wa Bahá'u'lláh, katika mifano itambulikayo, kumewavuka watu binafsi, familia na jamaa pana—kile kinachoshuhudiwa ni mjongeo wa umati kuelekea kitovu kimoja cha pamoja. Wakati mwingine, uhasama wa kale kati ya vikundi pinzani unaachwa nyuma, na baadhi ya miundo ya kijamii na taratibu za ukuaji zinabadilishwa kufuatana na mafundisho matakatifu.

18. Hatuwezi kufanya chochote zaidi ya kufurahia mno maendeleo haya ya kuvutia sana. Nguvu ya Imani ya Bahá'u'lláh ya kujenga jumuiya daima inadhihirika kwa uwazi zaidi, na huu ni msingi madhubuti ambao juu yake Mpango ujao wa Miaka Tisa utajengwa. Klasta zenye nguvu dhahiri, kama ilivyokuwa imetarajiwa, zimethibitisha kuwa bwawa la maarifa na rasilimali kwa ajili ya majirani zao. Na kanda ambamo kuna klasta zaidi moja kama hizo, zimeendeleza kwa urahisi zaidi nyenzo za kuchapuza ukuaji katika klasta baada ya klasta. Hata hivyo, tunajisikia kulazimika kusisitiza tena kwamba, maendeleo yamekuwa takriban ya ulimwengu mzima; tofauti katika maendeleo kati ya sehemu moja na nyingine ni ya kiwango. Uelewa wa pamoja wa jumuiya juu ya mchakato wa uingiaji kwa makundi na imani yake ya kuweza kuchochea mchakato huu katika hali yoyote, umeinuka kufikia ngazi ambazo zisingeweza kufikiriwa katika miongo iliyopita. Maswali ya kina ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu, na ambayo yaliwekwa bayana mnamo mwaka 1996, sasa yamejibiwa kwa uhakika na ulimwengu wa Kibahá'í. Kuna kizazi cha waumini ambacho maisha yake yote kemebeba alama za nyayo za maendeleo ya jumuiya. Lakini ukubwa wenyewe wa kile kilichotokea katika klasta hizo nyingi ambako safu za mbele za ujifunzaji zinaendelea kupanuliwa, umegeuza maendeleo muhimu katika mchakato wa uingiaji kwa makundi kuwa wa maana katika uwiano wa kihistoria.

19. Wengi watakuwa wanafahamu jinsi Mlinzi alivyogawanya Zama za Imani katika vipindi vinavyoongozana; kipindi cha tano cha Zama za Utungo kilianza mnamo mwaka 2001. Kile kisichojulikana sana ni kwamba Mlinzi pia alirejea mahususi kuhusu vipindi vya Mpango Mtakatifu, na hatua ndani ya vipindi hivyo. Ukiwa umesitishwa kwa miongo miwili wakati asasi za mahali na za kitaifa za Utaratibu wa Utawala zilipokuwa zinaanzishwa na kuongezewa nguvu, Mpango Mtakatifu uliobuniwa na 'Abdu'l-Bahá ulizinduliwa rasmi mnamo mwaka 1937 pamoja na mwanzo wa hatua ya kwanza ya awamu yake ya kwanza: Mpango wa Miaka Saba ambao Mlinzi aliukabidhi kwa jumuiya ya Kibahá'í ya Amerika ya Kaskazini. Kipindi cha kwanza kilifungwa baada ya hitimisho la Pambano la Miaka Kumi mnamo mwaka 1963, ambalo matokeo yake yalikuwa kwamba bendera ya Imani ilisimikwa kote ulimwenguni. Hatua ya pili ya kipindi cha kwanza cha Mpango wa Miaka Tisa, siyo chini ya Mipango kumi iiufuata mkondo wa mpango huo, Mipango ambayo inaanzia kipindi cha miezi kumi na mbili hadi kufikia miaka saba. Kwenye mapambazuko ya kipindi hiki cha pili, ulimwengu wa Kibahá'í tayari ulikuwa unashuhudia mwanzo kabisa wa uingiaji katika Imani kwa makundi ambayo yalikuwa yametabiriwa na Mwanzilishi wa Mpango Mtakatifu; katika miongo iliyofuata, vizazi vilivyojitolea wakfu vya waumini ndani ya jumuiya ya Jina Kuu Kabisa vilifanya kazi katika Shamba Takatifu la Mizabibu kukuza hali zilizohitajika kwa ajili ya ukuaji mpana sana uliodumishwa. Na kwenye msimu huu mtukufu wa Riḍván, ni mengi kiasi gani matunda ya kazi hizo! Jambo la kuwa na idadi ya kutosha inayotunisha shughuli za jumuiya inaposhika cheche ya imani na kuinuka haraka sana kutoa huduma kwenye ncha inayoongoza Mpango imesogea kutoka kuwa utabiri uliodumishwa na imani hadi kuwa

uhalisia unaotokea mara kwa mara. Maendeleo makubwa na yanayoonekana kama haya yanadai kuandikwa katika kumbukumbu ya Hoja. Kwa mioyo yenye kufurahi sana, tunatamka kwamba kipindi cha tatu cha Mpango Mtakatifu wa Bwana kimeanza. Hatua kwa hatua, kipindi baada ya kipindi Mpango Wake utakunjuka, mpaka mwangaza wa Ufalme utakapouangazia kila moyo.

20. Marafiki Wapendwa, hakuna mapitio ya shughuli ya miaka mitano ambayo yamehitimisha kipindi cha pili cha Mpango Mtakatifu, yangekamilika bila marejeo maalum kwa machafuko yaliyosindikiza mwaka wake wa mwisho na ambayo yangali yanaendelea. Makatazo ya mwingiliano wa watu binafsi ambayo yalipevuka na kupungua katika nchi nyingi kwenye kipindi hiki, yangeweza kuwa na mapigo makali kwa juhudi za pamoja za jumuiya, ambayo kupona kwake kungechukua miaka, lakini kuna sababu mbili kwa nini hili halikutokea. Moja ni utambuzi ulioenea kwa mapana wa wajibu wa Wabahá'í kutumikia jamii ya wanadamu, hususan katika kipindi cha hatari na shida. Pili ni kwamba uinukaji usio wa kawaida katika ulimwengu wa Kibahá'í kuonesha utambuzi huo. Pamoja na tajiriba ya miaka mingi ya kukubali ruwaza za utendaji wa kimpangilio, marafiki walitumia ubunifu wao na hisia ya kuwajibika juu ya hatari ambayo haikutarajiwa, na wakati huo huo wakihakikisha kwamba mbinu mpya walizokuza ziliwiana na muundo walioufanyia kazi na kuukamilisha katika mfuatano wa Mipango. Hii haimaanishi kupuuzia shida kubwa walizozipata Wabahá'í, kama wenzao katika kila nchi; walakini hata wakati wa kupitia taabu kali, waumini wameendelea kubaki makinikifu. Rasilmali zimeelekezwa kwa jumuiya zenye mahitaji, chaguzi ziliendelea popote palipowezekana, na katika kila hali asasi za Hoja zimeendelea kutekeleza majukumu yao. Zimekuwepo hata hatua za kijasiri zilizochukuliwa kwenda mbele. Baraza la Kiroho la Kitaifa la São Tomé na Príncipe litaundwa upya Riḍván hii, na mihimili mipya miwili ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu itainuliwa: Baraza la Kiroho la Kitaifa la Croatia, lenye makao makuu yake ndani ya mji wa Zagreb, na Baraza la Kiroho la Kitaifa la Timor-Leste, lenye makao makuu yake ndani ya Dili.

21. Na ndivyo Mpango wa Mwaka Mmoja unavyoanza. Kusudi na mahitaji yake tayari yamewekwa wazi katika ujumbe wetu uliotumwa kwenye Siku ya Agano; Mpango huu, ingawa mfupi, utatosha kuuandaa ulimwengu wa Kibahá'í kwa ajili ya Mpango wa Miaka Tisa ambao utafuata. Kipindi chenye uwezo maalum, ambacho kilianza miaka mia moja baada ya Ufunuo wa Nyaraka za Mpango Mtakatifu, punde kitahitimishwa kwa kutimia kwa miaka mia moja ya Kupaa kwa 'Abdu'l-Bahá, na kuweka alama ya mwisho wa karne ya kwanza ya Zama za Mtungo, na kuanza karne ya pili. Kikosi cha waaminifu kinaingia katika Mpango huu mpya katika kipindi ambamo jamii ya wanadamu, ikiwa imefundwa kupitia uanikaji wa madhaifu yake, kinaonekana kuwa na utambuzi mkubwa zaidi wa hitaji la ushirikiano kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za ulimwengu. Walakini, masalia ya tabia ng'ang'anivu za mashindano, maslahi binafsi, ubaguzi na ufinyu wa fikra, yanaendelea kuzuia mjongeo kuelekea umoja, licha ya idadi zinazoendelea kukua katika jamii za watu wanaoonesha kwa maneno na vitendo jinsi wao, pia, wanavyotamani kukubali kwa kiasi kikubwa zaidi umoja wa kiasili wa jamii ya wanadamu. Sisi tunasali ili familia ya mataifa iweze kufanikiwa kuweka kando tofauti zao kwa ajili ya maslahi ya wote. Licha ya wasiwasi unaoigubika miezi iliyo mbele, tunamsihi Bahá'u'lláh kufanya mathibitisho ambayo yamewadumisha wafuasi Wake kwa kipindi kirefu na kwa wingi

> zaidi, ili muweze kupelekwa mbele katika dhima yenu, utulivu wenu, bila kusumbuliwa na taabu za ulimwengu ambao hitaji lake kwa ajili ya ujumbe Wake uponyao ni kali zaidi kuliko wakati wowote.

Mpango Mtakatifu unaingia mwanzo wa kipindi kipya na hatua mpya katika historia. Ukurasa huu umegeuzwa.

*Nyumba ya Haki ya Ulimwengu*